

SOMO MAALUMU:

SISI WATEULE NDIYO WABADILISHA MAMBO YA

ULIMWENGU HUU PAMOJA NA MAZINGIRA YAKE.

MAANDIKO: RUM 8:28-30

1. UTANGULIZI:

- Tanzania ina katiba yake, na kila Raia anayetaka kuishi salama Tanzania lazima aheshimu Katiba ya Tanzania na afuate jinsi inavyoelekeza; akikiuka katiba ya nchi tu, mtu huyo atashughulikiwa na vyombo husika na ataishi kwa taabu sana kiasi cha kutamani ahame Tanzania!!
 - Tangu Joshua alipoambiwa na Mungu katika **Joshua 1:1-9** na kuambiwa mipaka ya nchi yao, na Israeli walipopata uhuru wao mwaka 1948, walisoma Torati na kuona mipaka yao na kuanza kuirudisha nchi yao kama Mungu alivyowapa; Nchi zote za Kiarabu zilijikusanya ili kupigana na Israeli ili kuwafuta kabisa kutoka katika uso wa dunia wasiwe nchi kabisa, jeshi la Waarabu lilipata jumla ya Wanajeshi 800,000-1,000,000, na jeshi la Israeli lilikuwa kama 60,000-80,000 tu; Jeshi hili dogo la Israel lilipiga nchi zote za Kiarabu na kufagia majeshi yao kabisa hadi Umoja wa Mataifa ukaingilia kati kwa kuisihi sana Israeli isimamishe vita ili isije ikafagia na Raia!! Mipaka ya Nchi yao kwamba aliwapa nchi hiyo na kuwaonyesha mipaka yao. **Kumb. 32: 30; Joshua 23: 9 – 10.**
2. Sisi ambao Yesu alitujua tangu asili na kisha akatuita, sisi ndiyo wabadilisha mambo pamoja na mazingira yake badala ya kuanza kulia hovy. **2Waf. . 4:1-7, Mated. 17: 5-6.**
- **Sisi kwa kweli Katiba yetu maalumu na nzuri mno tunayotakiwa kuifuata na kuiishi ni Biblia tukiwa hapa Tanzania au hata nje ya Tanzania na hata tutakoishi juu Mbinguni (Math 6:9-10).**

- Yesu Kristo katika kufundisha wanafunzi wake kuomba; akawataka waombe Ufalme wake uje hapa duniani kama ilivyo juu Mbinguni (Ufalme) maana yake utawala wake) na kama ambavyo Yesu Kristo alikuwa mbadilishaji mambo popote alipofika; kazi hiyo ameacha mikononi mwetu sisi tunaoamini. **Luk 7:11-18, Yoh. 11:39-45, Yoh. 2:1-11, Luk 5:1-11, Mark 5:25-34, Yoh. 9:1-32, Mark 4:36-41 n.k** na Manabii wake pamoja na Mitume wake aliowachagua na kuwaita na baadaye kuwatukuza nao walikuwa wabadili mambo pamoja na mazingira hatarishi. **2Waf. 7:1-20, (1-2, 18-20) 2Waf. 4:8-17, Dan. 3:15-29, Dan.6:10-27, (25-27) n.k**
- 3. Katiba yetu imeweka wazi kabisa mamlaka yetu na utawala wetu, tusiwe watu wa kulia na kulalamika hovy, tutafute wakati wote kuwa na moyo safi ili Bwana Yesu awe rafiki yetu, nasi tutafanya mambo makuu. **Mith 22:11, Math 5:8, Zab 51:10 n.k.**

- Mungu juu Mbinguni
- Nabii msemaji wa Mungu. **Kut 4:11-12**
- Watu wanaopokea maneno ya Unabii
(Katiba yetu) Biblia. **2 Petr 1:19, Ufun 22:18-19**

Maadamu tupo Tanzania, Nchi itaendelea kuwa salama, na Wamisri hawa tunawaona leo, hatutawaona milele kesho.
Kut. 14: 10 – 14. Amina.

Na
Ask. Dr. L. M. Mwizarubi
08/05/2022